
# Safari ya kuelekea Tokyo

## Mwongozo wa uadilifu kwa Mashindano ya Dunia ya Riadha ya 2025

(13-21 Septemba, Tokyo, Japan)




aiu_athletics

aiu_athletics

aiu_athletics

community@athleticsinetgrity.org

www.athleticsintegrity.org

Kijitabu hiki kinatoa maelezo muhimu kwa wanariadha wote na wafanyakazi wasaidizi wa wanariadha (ASP) wanaoshiriki katika Mashindano ya Dunia ya Riadha ya 2025 (WCH Tokyo 25).

Maelezo haya yatakusaidia kufuata Kanuni za Maadili na Sheria za Kupambana na Dawa za Kusisimua Misuli kabla, wakati wa, na baada ya WCH Tokyo 25.

Integrity Code of Conduct
Anti-Doping Rules

athleticsintegrity.org/road-to-tokyo

# Athletics Integrity Unit (AIU) ni nani?

Athletics Integrity Unit (AIU) ni idara huru iliyoundwa na Shirikisho la Riadha Duniani (World Athletics) ambayo husimamia masuala yote ya uadilifu – yanayohusu matumizi ya dawa za kusisimua misuli (doping) na yale yasiyohusu – katika mchezo wa riadha

## Sisi...

Hushirikisha
husaidia
huwezesha
hutetea
huelimisha
huwasiliana
hupima
huchunguza
hushtaki



# Nguvu ya Heshima

Kampeni ya Nguvu ya Heshima ilizinduliwa wakati wa Mashindano ya Dunia ya Budapest mwaka wa 2023 ili kuangazia nguvu iliyo nayo ya kujiheshimu, kuwaheshimu wengine na kuheshimu sheria, katika kulinda uadilifu wa mchezo wetu.

Tangu wakati huo, kampeni hii imekuwa na athari kubwa duniani kote na imepokewa vizuri na jamii ya riadha.

Katika WCH Tokyo 25, kampeni hii itaendelezwa ili kuangazia nguvu ya kuwaheshimu wengine kupitia matendo ya kila siku.

Hili litakuwa lengo la shughuli zetu za uhamasishaji katika WCH Tokyo 25, ambapo tunakualika uungane nasi ili kujadili maana ya nguvu ya heshima kwako na upate usaidizi wetu wa ana kwa ana na maelezo zaidi kuhusu mada zote za uadilifu.

**Kati ya tarehe 11-21 Septemba, utatupata katika Hoteli ya Shinagawa Prince (Hoteli ya Timu), Jumba la Annex, ghorofa ya 5 (5F), karibu na ukumbi wa kulia chakula (Prince Hall).**




Wajumbe wa Tume ya Wanariadha ya Shirikisho la Riadha Duniani, Aisha Praught-Leer na Dame Valerie Adams katika banda letu kwenye Mashindano ya Dunia ya Riadha ya 2023 mjini Budapest

# Mpangilio wa Anti-doping jijini Tokyo

**Kabla ya WCH Tokyo 25**

Ukiwasili Tokyo, unaweza kuchaguliwa kwa ajili ya vipimo vya “pre-competition”* katika hoteli ya Timu.

Ukichaguliwa, utaalikwa kwenda kwenye kituo cha kupima 'doping' (DCS) kilichowekwa mahali pa wazi katika hoteli ya Timu.

**Wakati wa WCH Tokyo 2025**

AIU itafanya vipimo uwanjani na katika maeneo mengine nje ya uwanja mkuu wakati wote wa mashindan

Unaweza kupimwa katika viwanja vya mashindano, hata kama ulipimwa kabla ya mashindano (pre-competition).

**Baada ya WCH Tokyo 25**

Unaweza kupimwa kama kawaida na AIU, Shirika la Kitaifa la Kupambana na Doping (NADO) la nchi yako (kama ADAK nchini Kenya), na NADO zingine ukiwa nje ya nchi.

# Kipindi cha Ndani ya Mashindano na Nje ya Mashindano
## (In-Competition and Out-of-Competition period)

Hata kama utatumia dawa ukiwa Nje ya Mashindano (out-of-competition), ikiwa dawa hiyo imepigwa marufuku Wakati wa Mashindano na ikapatikana kwenye sampuli yako (iliyochukuliwa Wakati wa Mashindano), unaweza kuadhibiwa.

Hii ni moja ya sababu kwa nini ni muhimu sana kwako kujua tofauti kati ya vipindi vya Ndani ya Mashindano na Nje ya Mashindano:

| Ndani ya Mashindano (In-Competition) | Nje ya Mashindano (Out-of-Competition) |
|---|---|
| Ni kipindi kinachoanza saa 23:59 (saa tano na dakika hamsini na tisa usiku) siku moja kabla ya Mashindano ambayo mwanariadha amepangiwa kushiriki, hadi mwisho wa Mashindano hayo na mchakato wa ukusanyaji wa sampuli unaohusiana na Mashindano hayo. | Kipindi kingine chochote ambacho si Ndani ya Mashindano. Hii inamaanisha nyakati zingine zote. |
| * Kabla ya Mashindano (Pre-Competition) ni kipindi kabla ya Tukio kuanza, kwa kawaida huanza unapowasili kwenye malazi ya tukio. Wakati huu, sheria za upimaji za Nje ya Mashindano ndizo hutumika. | |

# Orodha Haramu (Prohibited List)

Orodha Haramu ya WADA ya 2025 itatumika kwa WCH Tokyo 25. Orodha hii inajumuisha dawa na mbinu zote zilizopigwa marufuku Ndani na Nje ya Mashindano.

## Therapeutic Use Exemption (TUE)

TUE unakuruhusu kutumia dawa au mbinu iliyopigwa marufuku iwapo unaweza kutoa uthibitisho halisi wa kimatibabu ulioandikwa kwamba unaihitaji.

Wanariadha wote watakaoshiriki WCH Tokyo 25 wanachukuliwa kuwa wa 'Kiwango cha Kimataifa' na ni lazima wawe na TUE halali kabla ya kutumia dawa au mbinu iliyopigwa marufuku.

TUE ya sasa ambayo imeidhinishwa na NADO yako inahitaji kutumwa kwa AIU ili iidhinishwe au itambuliwe kabla ya tarehe 14 Agosti (siku 30 kabla ya kuanza kwa WCH Tokyo 25) kupitia: tue@athleticsintegrity.org.

Ikiwa utagundua unahitaji TUE, tuma maombi kwa AIU haraka iwezekanavyo ukifuata mchakato huu wa kutuma maombi. athleticsintegrity.org/know-the-process/therapeutic-use-exemptions.

# Taarifa za Mahali Ulipo (Whereabouts)

Katika WCH Tokyo 25, wanariadha walio katika Kundi Lililosajiliwa la Upimaji (RTP) lazima waendelee kuwasilisha taarifa za kina za mahali walipo kila siku.

Inasalia kuwa jukumu la mwanariadha kuhakikisha taarifa hizi ni sahihi na zimesasishwa wakati wote.

## Taarifa za Mahali Ulipo lazima zijumuishe:

- Malazi ya kila usiku
- Saa moja maalum ya kila siku (60-minute time slot)
- Ratiba ya mashindano
- Shughuli za kawaida (k.m., ratiba ya mazoezi)
- Ratiba ya safari

*Wanariadha wasio katika kundi la upimaji hawahitaji kuwasilisha taarifa za Mahali Walipo katika WCH Tokyo 25.*


| Vikumbusho Muhimu kwa Wanariadha wa Kundi la Upimaji Wanaoelekea WCH Tokyo 25 | |
|---|---|
| Kuelekea WCH Tokyo 25 | Ikiwa unasafiri kwa ajili ya matukio, mashindano ya kufuzu, au kambi za mazoezi, hakikisha taarifa zako za Mahali Ulipo zimesasishwa na ni sahihi. |
| Unapowasili Tokyo, kabla ya WCH Tokyo 25 kuanza | Sasisha taarifa zako za Mahali Ulipo kwa kuweka nambari ya chumba chako, ratiba za mazoezi na za mashindano, punde tu unapozipokea. |
| Wakati wa WCH Tokyo 25 | Hakikisha taarifa zako za Mahali Ulipo ni sahihi katika vipengele vyote. Fanya mabadiliko punde tu unapofahamu kuhusu mabadiliko hayo. |
| Kufuatia WCH Tokyo 25 | Wasilisha taarifa za Mahali Ulipo (whereabouts) kama kawaida. |

# Udanganyifu katika Mashindano

Ni jaribio lolote la kudhibiti matokeo ya mashindano au kubadilisha mkondo wa asili wa tukio la michezo, au sehemu yake.

Hii inaweza kujumuisha kubadilisha matokeo, kupanga matokeo, kubadilisha vifaa, ufisadi, kutojituma ipasavyo, au kusambaza taarifa za ndani.

Vitendo kama hivyo vinaweza kufanywa kwa lengo la kupata faida ya kifedha, faida ya kimichezo, au kutokana na shinikizo kutoka nje.



# Katika WCH Tokyo 25

FANYA: Ripoti jaribio lolote la kushawishiwa unalolifahamu haraka iwezekanavyo, ama kwa siri kupitia njia zetu za kuripoti, au ana kwa ana kwa mfanyakazi yeyote wa AIU.

FANYA: Shirikiana na uchunguzi wowote unaoendeshwa.

USIFANYE: Shiriki katika kipengele chochote cha kubadilisha matokeo katika WCH Tokyo 25 kwa manufaa yako au ya wengine.

USIFANYE: Toa, tafuta au pokea manufaa yanayohusiana na udanganyifu katika mashindano au aina nyingine yoyote ya ufisadi.

USIWEKE DAU kwenye shindano lako au shindano lingine lolote na USIMTAKE mtu mwingine kuweka dau kwa niaba yako.

USISAMBAZE taarifa za ndani (kama vile kumwambia mtu mwingine kuhusu jeraha la mwanariadha).

# Sheria za Viatu

Sheria za Viatu za Shirikisho la Riadha Duniani zinaeleza ni viatu vipi vinaweza kuvaliwa wakati wa kushindana. Viatu vilivyoidhinishwa vinaweza kuangaliwa hapa: certcheck.worldathletics.org

## Kabla ya WCH Tokyo 25

- Hakikisha unaangalia viatu vyako ili utendaji wako uweze kuhesabiwa!
- Huenda ukahitajika kujaza fomu ya kutangaza viatu ili kuthibitisha aina ya kiatu utakachotumia kushindana na kuthibitisha kuwa kiko kwenye orodha ya viatu vilivyoidhinishwa.
- Tuma maombi ya idhini ikiwa viatu vyako vinahitaji marekebisho kwa sababu za kimatibabu.

## Katoka WCH Tokyo 25

- USIVAE viatu vya majaribio au vilivyotengenezwa maalum.
- Unaweza kufanyiwa ukaguzi wa viatu kwa hivyo kaa na viatu vyako vya riadha baada ya shindano lako.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na rules@worldathletics.org au angalia maswali yanayoulizwa mara kwa mara.
Frequently asked questions

# Ulinzi (Safeguarding)

Kuunda mazingira salama na ya kukaribisha ambapo kila mtu anaheshimiwa na kuthaminiwa ndio kiini cha ulinzi.
Kila mtu ana jukumu la kushiriki kikamilifu katika kuzuia dhuluma, unyanyasaji au unyonyaji kutokea katika riadha.

## Kabla ya WCH Tokyo 25

**Wanariadha wote na ASP wanapaswa kusoma Sera ya Ulinzi ya Tukio na mfumo wake unaolenga kutekeleza mazingira salama na chanya kwa wote.**

## Wakati wa WCH Tokyo 25

Afisa wa Ulinzi wa World Athletics atakuwepo kusikiliza wasiwasi wowote wa kiulinzi unaoweza kuwa nao na kuhakikisha hatua zinazofaa zinachukuliwa:
safeguarding@worldathletics.org



# Timiza Wajibu Wako kwa Kuripoti

Uwe wewe ni mwanariadha au ASP, heshima uliyo nayo kwako mwenyewe, kwa wanariadha wengine na kwa sheria ni muhimu katika kutusaidia kuweka riadha safi, salama na ya haki.

Njia moja unayoweza kulinda uadilifu wa mchezo wetu ni kuripoti ukiukaji wa uadilifu - haijalishi ni mkubwa au mdogo kiasi gani. Taarifa hii inaweza kuwa muhimu sana katika kutambua ukiukaji wa uadilifu ndani ya mchezo wetu.

Mfumo wetu mpya wa kuripoti unatuwezesha kuwasiliana moja kwa moja na wale wanaotumia sanduku letu salama la kupokea ujumbe ili kushiriki wasiwasi wao kwa siri.

Mawasiliano haya ya pande mbili ni muhimu kwani tunaweza kupata uelewa kamili zaidi wa wasiwasi uliopo na kutoa mrejesho wenye maana.

## Unaweza kutoa ripoti bila kujitambulisha kwenye:

athleticsintegrity.org/make-a-report

Tunapaswa kuwajibika kwa uadilifu wa mchezo wetu na tuchukue kila fursa kujifunza kuhusu sheria na mifumo iliyopo ili kulinda uadilifu wa mchezo wetu.

Dame Valerie Adams
Mwenyekiti wa Tume ya Wanariadha ya Shirikisho la Riadha Duniani (Athletes' Commission)

